
Darasa la 1

Kitabu cha hadithi 1

Kiswahili

# ★ Fisi Mjinga

# ★ Chura na Kiboko



Tusome Early Literacy Programme

# Fisi Mjinga

*Mwandishi:* ***Stephen Kwoma***

*Mchoraji:* ***Simon Ndonye***

Hapo kale Fisi na Sungura walikuwa marafiki.

Marafiki hao waliishi pamoja.





Siku moja Sungura alienda kutafuta chakula.

Fisi naye alibaki akifagia nyumba.

Jioni Sungura alirudi nyumbani.

Sungura alileta asali nyingi.






Fisi alifurahia sana. Alitaka kujua Sungura alitoa wapi ile asali.

Sungura akamwambia kuwa alitingisha mzinga wa nyuki.

Siku iliyofuata Fisi alienda kutafuta chakula.

Aliona mzinga na akaanza kuutingisha.





Nyuki walitoka ndani ya mzinga na kumuuma Fisi.

Fisi alikimbia hadi nyumbani huku akilia.

Sungura alimwona Fisi akija mbio huku Nyuki wakimfukuza.

Sungura alimcheka Fisi.





Fisi alikasirika na kumfukuza Sungura kutoka nyumbani mwao.

Wanyama hawa hawakuishi pamoja tena.

## Maswali

1. Sungura alileta nini?
2. Kwa nini Nyuki walimfukuza Fisi?
3. Kwa nini Sungura alimcheka Fisi?

# Chura na Kiboko

*Mwandishi:* ***Flavia Nanzala***


*Mchoraji:* ***Simon Ndonye***


Hapo zamani, Chura na Kiboko walikuwa marafiki.

Wanyama hao walikuwa majirani.

Chura alikuwa na sauti nyororo.

Kiboko naye alikuwa na sauti nzito.





Siku moja, Kiboko alialikwa katika mashindano ya kuimba.

Aliogopa kushindwa kwa sababu ya sauti yake nzito.

Kiboko alimuomba Chura sauti yake nyororo.

Chura alimpa Kiboko sauti yake nyororo.


Kiboko alienda kwa mashindano akiwa na furaha.

Kiboko aliimba vizuri sana akawa mshindi.



Baada ya mashindano, Kiboko hakurudisha sauti ya Chura.

Kiboko alitoroka na kwenda kuishi majini.



Chura alimngoja Kiboko lakini Kiboko hakurudi.

Siku iliyofuata, Chura alienda mtoni kuchota maji.

Chura alimwona Kiboko mtoni.

Chura alimwambia Kiboko amrudishie sauti yake.

Kiboko akajificha ndani ya maji.

Tangu siku hiyo, Chura hulia majini akidai sauti yake.

## Maswali

1. Kiboko alimuomba Chura nini?
2. Kiboko alikuwa anaenda mashindano ya nini?
3. Kwa nini Chura hulia majini?

**Darasa la 1**

Kitabu cha hadithi 1

# ★ Fisi Mjinga

# ★ Chura na Kiboko

Vitabu vya hadithi vya **Tusome** vimeandikwa kwa ustadi wa hali ya juu ili kusaidia kuinua kiwango cha kusoma kwa wanafunzi wa darasa la 1 na la 2. Hadithi hizi zinawapa wanafunzi nafasi ya kufurahia hadithi na kuinua uelewa wa hadithi nje ya masomo ya kawaida darasani. Vitabu hivi vinaweza kutumiwa na yeyote anayejifunza Kiswahili. Tunashukuru kwa usaidizi wa SIL LEAD kwa mchango wao katika kuandika hadithi hizi. Ili kusaidia katika juhudi hii, hadithi hizi zimeandikwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Lugha rahisi kwa wanafunzi na sentensi zenye urefu unaofaa,
- Picha za kuvutia ambazo hazielezi hadithi kikamilifu lakini zinamwezesha msomaji kusoma zaidi ili aelewe hadithi,
- Hadithi za kufurahisha zenye maudhui na dhamira ambazo msomaji anayeanza kusoma ataweza kulinganisha na maisha yake ya kila siku,
- Vichwa vya hadithi ambavyo vinamwezesha msomaji kutabiri.

**Hadithi katika msururu huu ni:**

***Darasa la 1:***
- Fisi Mjinga **na** Chura na Kiboko
- Mchezaji Banda **na** Kisa cha Simba na Mbuni
- Faida za Ng'ombe **na** Siku za Wiki
- Kwa nini Mzee Kobe ana magamba **na** Jitu la Mtoni

***Darasa la 2:***
- Shujaa Musa **na** Mnyama Nimpendaye
- Mama Mzee na Nguruwe **na** Juma na Sungura
- Fisi na Mbuzi **na** Kuku na Mwewe Wakosana
- Sababu ya Paka Kupenda Kukaa Jikoni **na** Kwa nini Twiga ana Shingo Ndefu
- Safari ya Mombasa **na** Masaibu ya Musa

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.